



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA WANGING'OMBE



Simu 1: 0262784505
Simu 2: 0262784507
Barua pepe:
md@wangiwasa.go.tz
info@wangiwasa.go.tz

Km 5 kutoka Halali, Njiapanda
Barabara ya Iringa-Mbeya
Mji Mdogo wa Illembula
S.L.P. 317
MAKAMBAKO

MKATABA WA KUTHIBITISHA UBORA WA MABOMBA YA MAJI

MKATABA HUU Unafanyika leo tarehe 28 Aprili, 2022

BAINA YA

MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA WANGIN'GOMBE wa S.L.P 317,
MAKAMBAKO (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama Mwajiri) kwa upande
mmoja wa mkataba.

NA

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA) wa S.L.P. 54203
DAR ES SALAAM (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama Mto huduma) kwa
upande mmoja wa mkataba.

KWAMBA

Mwajiri anakusudia Mto huduma kufanya kazi ya kupima ubora wa mabomba
yatakayotumika katika mradi wa Uviko -19

MKATABA HUU UNASHUHUDIA HAYA YAFUATAYO:

1. MUDA WA KUANZA, UKOMO NA MAREKEBISHO.

- Mkataba huu ni wa siku 60 kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa mkataba huu .

- ii. Pasipo kuathiri masharti ya kifungu namba moja hapo juu, katika kipindi cha utekelezaji wa mkataba huu, pande husika zinaweza kukutana na kukubaliana kufanya mabadiliko katika kifungu au vifungu vya mkataba huu kwa kadili itakavyonekana inafaa.

2. WAJIBU WA MTOA HUDUMA.

- i. Mtoa huduma atahakikisha upimaji wa ubora wa bomba anaoufanya unakuwa bora kwa viwango vinavyoelekezwa .
- ii. Mtoa huduma atahakikisha anatekeleza kazi ya kupima ubora wa bomba kwa muda sahihi.

3. GHARAMA ZA MKATABA NA UTARATIBU WA MALIPO.

- i. Mtoa huduma atalipwa kutokana na kazi ya kupima ubora wa mabomba kama inavoonekana katika jedwali hapo chini.

Na	AINA YA BOMBA	AINA YA KIPIMO	IDADI	KIWANGO	GHARAMA
1.	HDPE $\frac{3}{4}$ "	HYDROSTATIC PRESSURE TEST	2	90,000	180,000/=
2.	HDPE $1\frac{1}{2}$ "	HYDROSTATIC PRESSURE TEST	2	90,000	180,000/=
3.	HDPE 2"	HYDROSTATIC PRESSURE TEST	2	90,000	180,000/=
4.	HDPE $2\frac{1}{2}$ "	HYDROSTATIC PRESSURE TEST	2	90,000	180,000/=
	JUMLA				720,000/=
	KODI 18%				129,600/=
	JUMLA KUU				849,600/=

4. MAJUKUMU YA MWAJIRI

- i. Kusimamia kazi inayotekelizwa na Mtoa huduma.
- ii. Kuhakikisha Mtoa huduma analipwa kwa wakati fedha za kazi alizofanya kama ilivyobainishwa kwenye mkataba huu
- iii. Kuhakikisha ubora wa kazi unafikiwa na kutoa taarifa ya kazi husika.

5. MATUKIO YASIWOTARAJIWA ENEO LA KAZI

- a. Tukio au jambo lolote litakalotokea wakati wa utekelezaji wa kazi ambalo halikutarajiwa na Mwajiri au Mtoa huduma na kama lipo nje ya uwezo wa pande zote mbili za mkataba huu na litakalopelekeea kuchelewa kwa kazi matumizi ya muda wa ziada kwa kazi iliyokwama, majadiliano na makubaliano yatafanyika kati ya pande mbili za mkataba ili kufikia maamuzi ya tukio lililojiteza ikiwa ni pamoja na utoaji wa ongezeko la muda la utekelezaji wa kazi ikibidi.
- b. Endapo Mtoa huduma atasababisha hasara/kutokana na uzembe katika utekelezaji wa majukumu yake atawajibika kulipia fidia kwa hasara iliyojitokeza na pia hatua za kisheria zitachukuliwa kwa ziada ya hasara hiyo.

6. KUSITISHWA KWA MKATABA

- a. Mwajiri atakuwa na haki ya kusitisha mkataba pale atakapoonaa au kuamini kwa namna yeyote ile Mtoa huduma atashindwa kukamilisha kazi ndani ya muda ulioainishwa, Mtoa huduma kushindwa kuendelea na kazi na Mtoa huduma kuonyesha udhaifu au uwezo mdogo wa kiufundi chini ya ule uliotarajiwa.
- b. Mkataba huu unaweza kusitishwa na upande wowote wa mkataba huu kwa kutoa taarifa ya maandishi ya siku kumi na nne (14) ya kusudio la kusitisha mkataba huu kama upande mwigine utashindwa kutekeleza mashariti ya mkataba huu.

7. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utatafsiliwa kwa kutumia sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

08. UTATUZI WA MIGOGORO

Kwamba iwapo utatokea mgogoro wowote ule kutohana na mkataba huu utatatuwa kwanza nje ya mahakama na msuluhishi ambaye atakuwa ni katibu Tawala wa Wilaya ya Wangin'gombe.

KWA USHUHUDA HUU, pande zote mbili zinaweka saini zao katika mkataba huu siku na tarehe kama ilivyo hapa chini:

1. KWA NIABA YA MAMLAKA YA MAJI:

Jina Mussa O. MASAI
Cheo N.D
Sahih ✓
Tarehe 28.4.2022
NIKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA
USAFI WA MIZINGIRI
WANGIN'GOMBE
SHAHIDI WA MAMLAKA YA MAJI
Jina EMMANUEL MAGESA
Cheo Ag. WSSM
Sahih ✓

MTOA HUDUMA

Jina JULIANNE MAFTEL
Cheo KAHU MEDEJA UCAMBESI
Sahih ✓
Tarehe 16/09/2012
NIKURUGENZI MKUU
KUWASO
SHAHIDI WA MTOA HUDUMA
Jina Joram SOSPETER ZACHARIA
Cheo REISA ESTERIA MULANDAMIZI
Sahih ✓